

Sehemu ya 8 Mpango wa Vocha ya Chaguo la Makazi



Idara ya Nyumba ya Jiji la Phoenix (City of Phoenix Housing Department)

Sehemu ya 8 Mpango wa Vocha ya Chaguo la Makazi Ufunguaji wa Ombi la Mapema kwa Orodha ya Wanaosubiri

UMEFUNGWA

Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu Kufunga

Pida ayuda si leer o hablar en inglés le resulta difícil.

如果在閱讀和說英語方面存在困難，請尋求幫助

Molimo Vas da zatražite pomoć ako teško čitate ili govorite engleski jezik

Vui lòng yêu cầu xin được giúp nếu khó đọc hoặc trở ngại khi nói tiếng Anh

يُرجى طلب المساعدة إذا كنت تواجه صعوبة في القراءة أو في التحدث باللغة الإنجليزية.

Je, kuna malipo ya kudumisha au kubadilisha ombi langu la mapema? Hapana, hakuna malipo ya kudumisha wala kubadilisha ombi lako la mapema wala kupokea Sehemu ya 8 Housing Choice Voucher.

Je, ni nini kitakachotendelea ombi langu la mapema wakati kipindi cha ombi la mapema kimefungwa? Maombi yote ya mapema yaliyokamilishwa yataweka kwenye orodha ya wanaosubiri kwa kutumia nambari nasibu iliyoundwa na tarakilishi. Orodha ya wanaosubiri si ya kuwahudumia wale waliotangulia kufika.

Je, Tovuti ya Watuma Maombi ni nini? Tovuti ya Watuma Maombi ni mahali utakapoangalia hali ya ombi lako la mapema na kubadilisha taarifa yoyote iliyobadilika kwenye ombi lako la mapema. Tovuti ya Watuma Maombi itafanya kazi kwa takribani siku 30 baada ya kipindi cha ombi la mapema kufungwa tarehe 26 Septemba, 2023, saa 7 jioni.

Je, nitajisajili vipi ili kuingia kwenye Tovuti ya Watuma Maombi? Takribani siku 30 baada ya kipindi cha ombi la mapema kufungwa tarehe 26 Septemba, 2023, saa 7 jioni, utajisajili kwenye Tovuti ya Watuma Maombi kwa kutumia nambari ya uthibitishaji uliyopokea ulipowasilisha ombi lako la mapema. Unaweza kujisajili kwenye tovuti ya MyHousing kwenye: phxhousing.myhousing.com. Ukipoteza nambari yako ya uthibitishaji, unaweza kuiomba kwa kuwasiliana na ofisi ya Idara ya Nyumba ya Jiji la



Sehemu ya 8 Mpango wa Vocha ya Chaguo la Makazi



Phoenix (City of Phoenix Housing Department, COPHD) Section 8 kwa nambari 602-534-1974, tuma barua pepe S8intake@phoenix.gov, au tutumie barua au tutembelee 830 E. Jefferson Street, Phoenix, AZ 85034.

Je, ni vipi ninavyoweza kuangalia hali yangu ya orodha ya wanaosubiri na kusalia kwenye orodha ya wanaosubiri? Lazima watuma maombi waarifu COPHD kuhusu mabadiliko yoyote ya anwani, nambari ya simu, anwani ya barua pepe au wanafamilia. Unapopokea barua kutoka COPHD kuhusu ombi lako la mapema, lazima ujibu kufikia tarehe iliyoorodheshwa katika barua, la sivyo ombi lako la mapema litaondolewa kwenye orodha ya wanaosubiri. Ili kubadilisha taarifa zako au kuangalia hali ya ombi lako la mapema, unaweza kutumia njia yoyote kati ya zifuatazo:

- Kwenye tovuti ya MyHousing katika Tovuti ya Watuma Maombi: phxhousing.myhousing.com. Tovuti ya Watuma Maombi inahitaji usajili na matumizi ya nambari ya uthibitishaji wa ombi la mapema. Usajili wa Tovuti ya Watuma Maombi na hali ya ombi la mapema vitapatikana takribani siku 30 baada ya kipindi cha ombi la mapema kufungwa.
- Piga simu kwa nambari 602-534-1974
- Tuma barua kwenye ofisi ya COPHD Section 8 huko 830 E. Jefferson St., Phoenix, AZ 85034
- Mkutano wa ana kwa ana wakati wa saa za kazi za kawaida (kwenye anwani ya COPHD Section 8 iliyo hapo juu)

Je, ni vipi ninavyoweza kuomba mabadiliko yanayofaa kutoka COPHD? Tafadhali piga simu 602-534-1974, kamilisha na uwasilishe ombi hili [la fomu ya mabadiliko yanayofaa](#), au tutumie barua au ututembelee 830 E. Jefferson Street, Phoenix, AZ 85034.

Ahadi ya Nyumba Sawa na Kutokuwa na Ubaguzi: Jiji la Phoenix halibagui kwa msingi wa mbari, kabila, jinsia, utambulisho wa jinsi, rangi, dini, hali ya ndoa, hali ya familia, asili ya taifa, umri, ulemavu, kizazi, chanzo cha mapato au mwelekeo wa kingono katika ufikiaji, usajili, au ajira katika mipango ya nyumba au shughuli. COPHD haibagui kulingana na Sheria ya Nyumba Sawa (Fair Housing Act), Sheria ya Title VI ya Haki za Raia (Civil Rights Act), Kifungu cha 504 cha Sheria ya Urekebishaji ya 1973 (Rehabilitation Act), au Title II ya ADA (Americans with Disabilities Act).

